JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L. P. 42325,
TEMEKE.
Barua Pepe: rbctemeke@pccb.go.tz.
Tovuti: www.pccb.go.tz

TEMEKE MEI, 2023

WALIMU TEMEKE WAMPONGEZA MKURUGENZI

KUSITISHA KUCHANGIA VYAMA VYA WAFANYAKAZI

Walimu ambao ni wanachama wa Chama cha Kuwalinda na Kutetea Haki za Walimu Manispaa ya Temeke wamempongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Temeke Mheshimiwa Elihuruma Mabelya kwa kusitisha makato ya kuchangia vyama viwili vya wafanyakazi ambavyo ni Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na Chama cha Kuwalinda na Kutetea Haki za Walimu CHAKUHAWATA.

Awali walimu hao waliwasilisha malalamiko yao TAKUKURU kwamba wamekuwa wakikatwa mishahara yao na kuchangia vyama viwili kinyume na k/f cha 61(1) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini namba 6 ya Mwaka 2004 ambacho kinampa mfanyakazi mamlaka ya kutoa kibali makato yake yaelekezwe kwenye chama cha wafanyakazi anachoona kinamfaa.

Kifungu hicho cha Sheria kikisomeka pamoja na Kanuni ya 37 ya Kanuni za Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini za Mwaka 2007 havikutafasiriwa vizuri na watendaji wa Manispaa ya Temeke kiasi kwamba walimu hao waliendelea kukatwa asilimia 2% ya mishahara yao na kupelekwa CWT wakati walishajiondoa kwenye chama hicho na walistahi kukatwa kupitia CHAKUHAWATA pekee.

Kupitia kazi za uzuiaji rushwa kwa maana ya dhana ya TAKUKURU Rafiki na kwa kuzingatia k/f cha 7 Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na 11/2007 tulimshauri Mkurugenzi kuhusu kadhia hiyo ambayo imekuwa ikiwapata walimu hao na baada ya kupata ushauri huo alisitisha mara moja makato kwenda CWT kwa kuwa hakuwahi kutoa

maelekezo ya makato hayo. Pamoja na hili, TAKUKURU imeendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na Kuzuia, Kueleimisha na Kupambana na Rushwa kama ifuatavyo:-

UZUIAJI RUSHWA

Katika eneo la UZUIAJI RUSHWA, TAKUKURU Mkoa wa Temeke tulifanya ufuatiliaji wa mradi wa matumizi ya mikopo ya asilimia kumi ya mapato ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na kubaini kuwepo dosari mbalimbali kwa pande zote mbili ambazo ni **wakopaji** na **mkopeshaji** (Manispaa ya Temeke). Dosari zilizobainika kwenye mikopo hiyo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

- Baadhi ya vikundi kupewa mikopo isiyo kidhi malengo ya wanakikundi ambayo yaliwekwa kwenye andiko lao. Kwa mfano kikundi kinaomba mkopo mkubwa (sh. 60,000,000/=) wakiwa na matarajio ya kufungua mradi mkubwa kama vile duka kubwa mathalani duka la kuuza vifaa Tiba na kulifungua sehemu sehemu yenye mzunguko mkubwa wa biashara. Lakini walipewa sh. 27,000,000/=tu, ambazo hazikukidhi mahitaji na malengo ya wanakikundi na biashara yao.

- Baadhi ya vikundi kubadilisha biashara baada ya kupata mkopo, kwa mfano kikundi kinachukua mkopo wa fedha nyingi mathalani Tsh. 21,355,000/= kwa ajili ya kuuza na kusaga nafaka, lakini baada ya mkopo hawanunui mashine ya kusaga nafaka na badala yake, wananunua nafaka na kwenda kuzisagisha kwa wafanyabiashara wengine wenye mashine hizo.

Hata hivyo, vikundi hivi baada ya kuona nafaka zimepanda bei, walibadilisha biashara wakawa wanauza bidhaa nyingine tofauti andiko lao, wengine walikopa fedha za kikundi na kwenda kufanya biashara binafsi na wengine walifanya matumizi yao binafsi. Mwisho wake ni kwamba unakuta hakuna biashara ya kikundi inayoendelea kufanyika bali inakufa.

Katika hatua nyingine, tumefuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo **10** yenye thamani ya Sh. **14,423,405,163.70** Katika ufuatiliaji huo, jumla ya miradi **06** yenye thamani ya Sh.

9,388,171,494/= ilibainika kuwa na mapungufu kama inavyoonekana katika jedwali.

SN	JINA LA MRADI NA THAMANI	YALIYOBAINIKA	HATUA
1.	Ujenzi wa madarasa 32 shule ya sekondari Lumo, wenye thamani ya **Shs 1.6 BILIONI**	i. Ucheleweshaji wa malipo kwa mafundi. ii. Mafundi kugoma kufanya kazi.	Wahusika walishauriwa kuhakikisha wanatoa malipo ya mafundi kwa wakati.
2	Ufuatiliaji wa mradi wa matumizi ya asilimia kumi unafanywa na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke sh. 3,042,203, 550/=	i. Kutoa mikopo isiyokidhi mahitaji ya wanakikundi. ii. Wanakikundi kufanyia mkopo biashara binafsi. iii. Kushindwa kurejesha mkopo.	Uchambuzi wa mfumo unaandaliwa ili kufanya kikao cha pamoja kwa lengo la kuondoa changamoto hizo.
3	Ufuatiliaji wa mradi wa matumizi ya asilimia kumi unafanywa na Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni sh. 4,203,283,972/=	i. Ucheleweshaji wa marejesho ya mkopo. ii. Kukosekana kwa elimu kuhusu malengo ya mkopo.	Uchambuzi wa mfumo unaandaliwa ili kufanya warsha kwa ajili ya kuweka malengo na namna ya kuondoa changamoto hizo.
4	Ufuatiliaji wa ujenzi wa nyumba za Walimu shule ya Sekondari Pembamnazi Halmashauri Ya Manispaa ya	i. Mradi upo nje ya muda ukilinganisha na mkataba	Ushauri umetolewa kuwa miradi kama hii itekelezwe kwa njia ya Force Account kwa

	Kigamboni zenye thamani ya sh.114, 683,972/=	ulioingiwa baina ya fundi na Manispaa (mradi ulitakiwa kukamilika mwezi Machi 2023. ii. Upotevu wa fedha za wananchi unaotokana na kubadilishwa kwa mawanda ya mradi. iii. Upimaji wa ubora wa vifaa vya ujenzi (Material Testing) Haukufanika.	kuwa itatekelezwa kwa kufuata matakwa ambayo yanajieleza na kuhitaji kutumia Force Account kama kifungu cha 64 (5) cha manunuzi ya Umma (*PPA, 2011*) kinavyoeleza.
5	Mradi wa ujenzi wa madarasa 20 shule ya sekondari Nzasa kilungule wenye thamani ya sh. 400,000,000/=	i. Mbao za milango zimetofautiana, kuna (MDF na Hardwood). ii. Mlango mmoja ni mfupi.	Fundi ameshauriwa kubadilisha milango kwa kuweka milango ya mbao za Hard wood na siyo kuchanganya na mbao za MDF.
6	Ufuatiliaji wa mradi wa ukarabati wa vyumba 3 vya madarasa shule ya msingi Nzasa Sh.28, 000,000/=	i. Malipo kwa mafundi yanachelewa.	Ushauri umetolewa kwa Manispaa ya Temeke mafundi walipwe kwa wakati. Ufuatiliaji unaendelea.

UCHAMBUZI WA MIFUMO

TAKUKURU (M) TEMEKE imefanya, chambuzi za mifumo ikiwa na lengo la kubaini mianya ya Rushwa ambayo inaweza kupelekea vitendo vya Rushwa kutokea na kushauri Taasisi husika namna bora ya kurekebisha mapungufu yaliyobainika kwenye mifumo.

Kwa kipindi **cha Januari hadi Machi 2023,** TAKUKURU (M) TEMEKE imefanya uchambuzi wa mfumo unaohusu usimamizi wa mazao ya misitu katika Halmasahuri ya Manispaa ya Kigamboni. Lengo kuu la uchambuzi huu ulikuwa ni kuchunguza hatari au mianya ya rushwa katika usimamizi wa mazao ya Misitu katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni.

Katika chambuzi za mfumo huo yafuatayo yalibainika: -

SN	MFUMO	YALIYOBAINIKA	MAKUBALIANO
1	Mfumo wa usimamizi wa mazao ya misitu.	1. Kukosekana kwa vizuizi katika Wilaya ya Kigamboni. 2. Wananchi kutokuwa na elimu ya kutosha ya sheria zinazohusika katika kutunza na kuvuna mazao ya misitu/miti iliyopo katika maeneo mbalimbali ndani ya Manispaa.	1. Vizuizi viwekwe ili kuokoa mapato yanayopotea 2. Doria ifanyike mara kwa mara 3. Elimu itolewe kwa wadau wote wa mazao ya misitu ili wajue taratibu zinazotumika katika kuvuna miti/misitu ambayo ipo katika maeneo yao.

TAKUKURU Rafiki

TAKUKURU Rafiki ni program iliyoundwa kwa lengo la kumfikia kila Mwananchi katika kata ambapo utekelezaji wake ni kuibua kero na kushirikiana na wadau husika kwenye sekta zenye changamoto na kuzitafutia majibu kwa pamoja. Katika kutekeleza program ya TAKUKURU Rafiki, ofisi ya TAKUKURU (M) TEMEKE (Temeke na

Kigamboni) kwa kushirikiana na wadau kutoka kwenye sekta mbalimbali imeweza kufika kwenye maeneo yafuatayo: -

Kero zilizopokelewa na kuchukuliwa hatua mbalimbali ni kama ifuatavyo;

SN	SEKTA	IDADI YA KERO	HATUA ZILIZOCHUKULIWA	
			VIKAO NA WANUFAIKA	VIKAO NA WATOA HUDUMA
1	Barabara	1	Wananchi wa **KATA YA KIBADA (W) Kigamboni** inayojumuisha mitaa 6 ambayo ni Kiziza, Sokoni, Kichangani, Nyakwale, Kifurukwe na Uvumba. Kero ni barabara ya kwenda Mizimbini Sekondari na Mizimbini Shule ya Msingi hazipitiki na zina madimbwi makubwa ambayo ni hatari kwa usalama wa wanafunzi wa shule hizo tajwa.	**TARURA** imeandaliwa barua kupelekwa ili kuomba muda wa kukaa na uongozi wa TARURA ili kupata ufumbuzi wa kero tajwa.
2	Barabara	02	Wananchi wa Kata ya Chamazi:- 1. Bar ni nyingi chamazi, tabia za uovu zimezidi kwa vijana wetu. 2. Wafanyabiashara wadogo wadogo eneo la Mbande wananyanyaswa sana kiasi cha kuombwa pesa, yaani kama hauna pesa hufanyi biashara.	Kero zote zimewasilishwa kwa mtoa huduma.
3	Afya	1	Wananchi wa **KATA YA KIBADA (W) Kigamboni** inayojumuisha mitaa 6 ambayo ni Kiziza, Sokoni, Kichangani, Nyakwale, Kifurukwe na Uvumba. Kero - ukosefu wa dawa zahanati ya Kibada na majibu mabaya ya watoa huduma.	Barua kwenda **Zahanati ya Kibada** imeandaliwa ili kupata muda wa maafisa wa TAKUKURU na uongozi wa zahanati hiyo kujadili na kuona njia njema ya kutatua kero hiyo inapatikana.
4	Elimu	1	Wananchi wa **KATA YA KIBADA (W) Kigamboni** inayojumuisha mitaa 6 ambayo ni Kiziza, Sokoni, Kichangani, Nyakwale, Kifurukwe na Uvumba. Kero - Madarasa na madawati ya Shule ya msingi	Barua ya kwenda shule hizo zenye changamoto zimeandaliwa ili kupata muda wa kwenda kujadili na

			Kibada na Mizimbini hayatoshi.	uongozi wa shule hizo.
5	Elimu	11	Wananchi wa Kata ya Kilungule (W) Temeke ziliibuliwa kero zifuatazo:- Katika kata tunatatizo la watoto wakike wadogo kubakwa. a. Tunaomba kujengewa shule ya kata ya Kilungule. b. Watoto kutoa pesa za mitihani kwa kila siku, pia mitihani ya kufunga shule wazazi tunalipishwa 1200 c. Watoto katika shule ya msingi wasipotoa michango na kukosa pesa ya chakula wanachapwa na walimu wao d. Kudaiwa fedha kwa Huduma ya kuandikisha na kuhamisha mtoto shule. e. Mtoto anapokosa pesa ya mtihani shuleni anarudishwa nyumbani f. Huduma sio nzuri ya elimu walimu wamerudisha masomo ya jioni g. Shule hazina uwanja wa michezo h. Watoto kukaa chini darasani i. Wenye viti wa serikali za mitaa pamoja na Kamati za shule wanashirikiana na walimu na kuanzisha michango mashuleni ikiwemo mchango wa chakula,tuition, mitihani kila siku ni michango hatuna pesa, tunaomba ufafanuzi wa elimu bure j. Hatuna taarifa ya matumizi ya pesa ya Tamisemi inayotolewa kwa ajili ya michezo	Kero zote zimewasilishwa kwa mtoa huduma.
6	Elimu	15	Wananchi wa Kata ya Yombo Vituka (W) Temeke ziliibuliwa kero zifuatazo:- a. Ukarabati majengo ya shule zetu. b. Mtoto kupata namba ya	Kero zote zimewasilishwa kwa mtoa huduma.

			uhamisho pindi mzazi anaposhindwa kupa ada shule ya private Kwenda ya serikali. c. Watoto hawasomi kila siku wala hawaandiki Je? Watafauluje? d. Wanafunzi wa shule ya vituka ni wengi sana kwenye madarasa yao wanahatarisha Maisha yao je? Mnatusaidiaje. e. Tukarabatiwe majengo ya shule baadhi yameanza kuchakaa rangi. f. Ufungaji wa shule za awali ambao hadi sasa Watoto hawana pakusomea kwa sababu shule hizo zimefungwa taarifa za kuomba tenda katika mradi wa shule ya Lumo hazikuzingatia muda wa kuomba. g. Hatu taarifa za ujenzi madarasa ya Lumo Sekondari, taratibu za kuhamisha na kuhamia kwa Watoto Lumo Sekondari zimekuwa na ukwamishaji bila kujali hali yam toto au mzazi/mlezi. h. Michango ni mingi ufundishaji mdogo mashuleni. i. Watoto wetu wansoma mbali wakati shule yetu ya Lumo Sekondari ina nafasi kubwa. j. Kwa nini michango mashuleni imekuwa mingi? Na wakati huo huo hali zetu zinajulikana ni ngumu. k. Kelele za Bar zilizo karibu na shule mfano montifoti wakati wa usiku ni usumbufu sana, mfano sunset, Sawi, Jambo na Mandela wanaongoza kupiga mziki kwa sauti ya juu Monday to Monday. l. Michango mashuleni imezidi mfano mchango wa ulinzi, uji, mafagio na ada ya mitihani ya kila wiki na kila mwezi ni kero kubwa sana. m. Tunadaiwa hela ya twisheni kila siku shule ya buza hii ni kero kubwa sana. n. Watoto wetu wasipotoa hela ya mitihani wanapigwa sana mashuleni Je? Hii ni sawa. o. Hatuna shule ya kata mtaa wa sigara,	
7	Elimu	07	Wananchi wa Kata ya Chamazi (W) Temeke ziliibuliwa kero zifuatazo:- 1. Walimu shule ya Misingi Rufu kuchukua fedha kwa wazazi kwa kisingizio cha mitihani 2. Mashuleni michango ni mingi pamoja na kuwalipia waalimu ziada 3. Shule ya msingi Kisewe madarasa ni	Kero zote zimewasilishwa kwa mtoa huduma.

			machache watoto wanakaa chini 4. Ahadi ya diwani ya kutujengea mtaro bado hajatimiza pamoja na kutujazia kifusi katika barabara ya kuelekea shule. 5. Kuchelewa kujengewa shule mtaa wa Kiponza wakati eneo wanalo ili kuepukana na wingi wa wanafunzi wengi mno kupita kiasi 6. Michango mingi katika shule zetu za kata ya Chamazi ikiwemo Rufu, Mbande, Kisewe • Walimu shule ya Misingi Rufu kuchukua fedha kwa wazazi kwa kisingizio cha mitihani • Walimu shule ya Msingi Mbande wanatoza michango isiyo ya lazima pamoja na michango ya majaribio • Wanafunzi shule ya msingi mbande wanasahihishiwa masomo yao kwa kutozwa fedha, mwalimu anasubiri wakati wa kukaribia kutoka shule ndo anasahihisha watoto wanapanga mstari anatoa sh. 100 anasahishiwa akiwa hana anambiwa akae pembeni asubiri hadi mwalimu amalize kusahihisha ndo aidha akupe adhabu sasa watoto wqengine wadogo na wanarudi kwa makundi kuepuka watu wabaya njiani sasa wenzake wanamuacha hii hali sio nzuri • Michango ya rambirambi shule ya Msingi Mbande ni mingi mno anafiwa mtoto wa darasa la 3 anachangiwa shule nzima hizo pesa kwanza tunahakika gani kama zinafika, pia wakati mwengine mtoto huyu anakuja anasema mtoto aliyefiwa wa darasa la tatu mwengine anasema la tano kwaiyo kuna uwezekano mkubwa siku Mwalimu akiwa hana pesa anasingizia mtoto kafiwa mana taarifa zinazotoka sio rasmi kwa wazazi lakini sie wazazi tunawatoto zaidi ya mmoja sasa kutoa pesa inakuwa ngumu na usipotoa mtoto anapigwa. 7. Shule ya msingi Kisewe madarasa ni machache yapo 20 Wanafunzi zaidi ya elfu nne 4000	
8	Maji	1	Wananchi wa **KATA YA KIBADA (W) Kigamboni** inayojumuisha mitaa 6 ambayo ni Kiziza, Sokoni, Kichangani, Nyakwale, Kifurukwe na Uvumba. Kero - hakuna huduma ya maji Kibada ya DAWASA	Barua imeandaliwa kwenda Idara ya maji Wilaya kujadili ni lini wataleta huduma za maji

			mpaka mwananchi achimbe kisima chake.	Kibada.
9	Maji	09	Wananchi wa Kata ya Kilungule (W) Temeke ziliibuliwa kero zifuatazo:- a. Visima vya maji vipo lakini hawafaidiki na huduma hiyo b. Kisima cha kwa Mzungu pesa imetolewa fedha za c. Jimbo lakini hadi leo hatujui hatma yake yaani hakifanyi kazi hakuna umeme. d. Dawasa maji ya mgao na sehemu kubwa ya kata yetu hakuna maji ya DAWASA e. Maji machafu yanasambaa kwenye miundo mbinu f. Bomba limewekwa maji hayatoki g. Watoa huduma wa Dawasco wanatoa kauli chafu h. Maji tunayotumia sio rafiki kwa binadamu yaani ni ya chumvi i. Mabomba ya Dawasco hayatoi maji	Kero zote zimewasilishwa kwa mtoa huduma.
10	Maji	11	Wananchi wa Kata ya Yombo Vituka (W) Temeke ziliibuliwa kero zifuatazo:- a. Miundo mbinu shida watu wengi hawana maji ya dawasco, sehemu zingine mabomba yamepita ila wao hawajawekewa maji. b. Bei za maji ya dawasco ni sh. 3000/= hadi 2,500/= kwa unit, tunaomba kujua bei rasmi ni shilingi ngapi. c. Mabomba ya dawasco yakipasuka mafundi wanatuomba pesa. d. Mtaa wa machimbo mabomba hajawekewa. e. Maji yanatoka si kwa wakati yanatoka kwa kukatika katika wakati mwengine unakaa siku tatu hatuna maji. f. Wanaomba wasambaziwe maji kwa wingi (dawasco). g. Wanakisima chao chamzambalauni wanaomba kichimbwe ili wananchi wapatiwe maji. h. Wanaomba punguzo la maji bill	- Kero zote zimewasilish wa kwa mtoa huduma.

			kubwa. i. Vituka hawana maji safi hadi sasa licha ya kusambaza mabomba wanaomba juhudi iongezwe maji yawafikie. j. Kila ikifika tarehe 20 ya mwezi k. tunadaiwa tulipe bili ya maji na usipokuwa nayo vitisho ni vingi ikiwemo kukatiwa maji, tunaomba hili liangaliwe mana wengine hizo terehe hata mshahara tunakuwa hatujapata	
11	Maji	10	Wananchi wa Kata ya Chamazi (W) Temeke ziliibuliwa kero zifuatazo:- 1. Maji ya Dawasa hakuna kabisa kwa wananchi walio wengi wa kata ya Chamazi Mtaa wa Dovya, Rufu wananchi wa kawaida wanapata tabu sana 2. Kero ya maji tunanunua UNIT moja Tshs.3000, tunaomba Dawasa ilete maji ya Serikali 3. Visima tulivyochimbiwa kwa msaada kutoka TASAF kwa matumizi ya kaya masikini vimechukuliwa na Dawasa na kuwatoza pesa walengwa pia bili ni kubwa sana. 4. Tunataka maji ya Dawasa tunatumia maji sio salama 5. Dawasa kuna tatizo la kubambikia bili 6. Tuliambiwa tutapata maji mpaka leo hatujaletewa 7. Chamazi hatuna maji ya Serikali tukiwauliza majibu yake hayapo ya kuridhisha na wakumuuliza hayupo 8. Kisewe tuliambiwa mradi utakamilika mwezi wa pili mpaka leo hatujaona maji 9. Hayapatikani kwa muda mwingi 10. Mtaro unapokea maji kutoka maeneo yote Mbande Dawasa kwenye eneo hili hawajatuletea maji	- Kero zote zimewasilish wa kwa mtoa huduma.
12	TRA	4	Wananchi wa Kata ya Chamazi (W) Temeke ziliibuliwa kero zifuatazo:- a. Mzunguko ni mkubwa katika kukata leseni na kulipa kodi, tuwe na kituo kimojwapo huduma zote zimalizwe hapo za TRA, na ukataji wa leseni au ziletwe katani b. Wafanya biashara wengi wa kilungule na mitaa yake hawana leseni za kufanyia biashara na TIN sababu ya kutokuwa na elimu ya biashara	- Kero zote zimewasilish wa kwa mtoa huduma

			c. Malipo ya kodi kwa wafanyabiashara ni makubwa na ndo yanakwamisha ulipaji wa kodi na ukataji wa leseni pia hali ya biashara kwa sasa sio nzuri. d. TRA wanatumia mabavu kudai kodi, hatuna elimu ya ulipaji wa kodi waje katika Kata kutuelimisha	
13	Nishati	07	Wananchi wa Kata ya Kilungule (W) Temeke zilliibuliwa kero zifuatazo:- a. Tanesco kutofika kwa wakati pindi huduma inapohitajika (kutoa huduma kwa wakati) b. Kukatika kwa umeme mara kwa mara c. Kuongezeka kwa gharama za umeme d. Vishoka ni wengi Kilungule wanatapeli wananchi wakidai kuwasaidia e. Kutoa hela bila kupewa risiti f. Kutoa taarifa ya kukatika kwa umeme kunapelekea vitu kuharibika na kuungua. g. Namba ya simu ya dharula kila ikipigwa inasema inatumika haipatikani	Kero zote zimewasilishwa kwa mtoa huduma.
14	Nishati	02	Wananchi wa Kata ya Yombo Vituka (W) Temeke zilliibuliwa kero zifuatazo:- a. Umeme kukatika mara kwa mara bila ya tahadhari na kusababisha hasara kwa wafanya biashara na watu wa kawaida nyumbani. b. Tanesco na Sigara wamejenga na kuziba barabara kusababisha wananchi kukosa kwa kupita.	- Kero zote zimewasilish wa kwa mtoa huduma.
15	Nishati	06	Wananchi wa Kata ya Chamazi (W) Temeke zilliibuliwa kero zifuatazo:- 1. Umeme kukatika mara kwa mara katika kata ya Chamazi hasa rufu kiasi cha kusababisha hasara hivyo tunaomba kata yote iwekewe umeme wa uhakika. 2. Uhaba wa usambazaji wa umeme eneo la kiponza na soko la Mbuyuni	Kero zote zimewasilishwa kwa mtoa huduma.

			3. Hakuna utaratbu mzuri wa kutoa huduma kwa mtu aliyelipia kuwekewa LUKU, Mtu anayelipa awekewe umeme kwakutumia fomula ya FIFO lakini kwa utaratibu uliopo unatuumiza mana kuna amelipa leo anawekewa na sie ambao maombi yetu yapo huko kitambo hatuwekewi. 4. Tanesck watoe taarifa ya kukatika umeme au kama kuna matengenezo itolewe taarifa ili kuepusha hasara zinazotupata. 5. Gharama zakuwekewa umeme zipunguzwe au tuingiziwe bure kisha wakatwe kwa kadiri wanavyonunua 6. Urasimu umezidi katika usambazaji wa umeme	
16	Ardhi	1	Wananchi wa **KATA YA KIBADA (W) Kigamboni** inayojumuisha mitaa 6 ambayo ni Kiziza, Sokoni, Kichangani, Nyakwale, Kifurukwe na Uvumba. Kero ni **warasimishaji makazi** wanachukua fedha za wananchi na baada ya hapo hawaonekani tena na kazi haifanyiki.	Barua imeandaliwa kwenda idara ya ardhi wilaya ili kukutana nao.
17	NIDA	02	Wananchi wa Kata ya Chamazi (W) Temeke ziliibuliwa kero zifuatazo:- a. Nida wanasumbua kupata vitambulisho, sasa hivi tuna mwaka wa tatu (3) tunapewa namba tu b. NIDA Temeke wanasumbua sana	Kero zote zimewasilishwa kwa mtoa huduma.
18	Polisi	1	Wananchi wa **KATA YA KIBADA (W) Kigamboni** inayojumuisha mitaa 6 ambayo ni Kiziza, Sokoni, Kichangani, Nyakwale, Kifurukwe na Uvumba. • Kero ni kuombwa rushwa kwa ndugu wa mtuhumiwa ambaye anatakiwa kupewa dhamana na isipotoka wanamnyima haki ya dhamana au wanambadilishia kesi yake ya awali na kumpa tuhuma mbaya zaidi ya kutengenezwa. • Ukienda kumshitaki mtu au ukamkamata mtu na kumfikisha kituo cha polisi unatoka tu getini na	Barua imeandaliwa kwenda kwa mkuu wa kituo cha polisi Kibada ili kuona upatikanaji wa tuhuma hii au kero hii kwa wananchi.

			mtuhumiwa unamuona na yeye ameachiliwa. Imepoteza kabisa imani ya wananchi kwa jeshi la polisi.	

UELIMISHAJI UMMA

Katika uelimishaji umma, Ofisi ya TAKUKURU (M) TEMEKE imefanya kazi za kuimarisha klabu za wapinga Rushwa kwenye shule za sekondari, msingi na vyuo, imefanya mikutano ya hadhara na imefanya semina kwenye idara mbalimbali na vipindi vya Redio na katika kushiriki maonyesho. Lengo kubwa ni kuzidi kuielimisha jamii kuhusu Rushwa na kuifanya jamii iweze kujua wajibu wake na namna inavyoweza kuisaidia Serikali kuwa mstari wa mbele katika kuzuia Rushwa hasa kwenye miradi ya maendeleo ambayo inatekelezwa kwa fedha nyingi kutoka Serikalini.

Kazi zilizofanyika kwa kipindi cha Januari hadi Machi 2023 ni kama ifuatavyo:-

NA	KAZI	IDADI	HALMASHAURI	MAENEO	KAZI
1	Semina	19	Temeke na Kigamboni	Watumishi - Tanesco, NGOs, MSD,Utalii,Afya,PSSSF, Viwanda,Ardhi na Mamlaka ya usimamizi wa wanyamapori (TAWA)	Kuzuia vitendo vya rushwa katika sekta husika.
2	Mikutano/Mijadala ya wazi	10	Temeke na Kigamboni.	Wananchi, Wajasiriamali, Wasanii, Wanahabari, Wanufaika wa Mikopo ya 10% na madereva bodaboda na bajaj.	Kukuza uungwaji mkono na wananchi kwenye uzuiaji Rushwa. Kuongeza ushiriki wa wananchi katika mapambano dhidi ya Rushwa.
3	Kuimarisha klabu za	11	Temeke na Kigamboni	Vijana-Vyuo, sekondari na Msingi	Kujenga uzalendo na ujasiri wa

	wapinga rushwa				kukemea vitendo vya rushwa.
4	Taarifa kwa vyombo vya habari	1	Temeke na Kigamboni.	Vyombo vya Habari, wananchi na watumishi wa TAKUKURU	Kuongeza wigo wa kupasha habari
5	Makala	3	Temeke na Kigamboni.	Wananchi	Kuhabarisha umma kuhusu kazi zilizofanyika zenye tija zaidi.
6	Vipindi vya redio	2	Temeke na Kigamboni.	Redio uhuru na Redio Upendo	Kuhabarisha umma kuhusu Programu ya TAKUKURU Rafiki.
7	Maonyesho	2	Temeke na Kigamboni	Wiki ya sheria viwanja vya Hakimu Mkazi Kisutu	Kuhudumia wananchi waliotembelea banda la TAKUKURU katika viwanja hivyo.

UCHUNGUZI NA MASHTAKA

Pamoja na kufanya mikakakati na juhudi za **KUZUIA RUSHWA na Uelimishaji umma,** bado wapo wananchi wachache ambao wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya rushwa. Hivyo katika kipindi husika, tumepokea **malalamiko mbalimbali 54 (46 yanahusu rushwa na 8 yasiyohusu rushwa)**

Malalamiko **yaliyohusiana** na vitendo vya Rushwa yalijumuisha sekta zifuatazo:-

NA.	SEKTA	IDADI
1	Manispaa ya Temeke	
	Utumishi	01
	Ugavi	09
	WEO	04
	TAMISEMI	02
	Ardhi	09
	Afya	01
	Elimu	02
2	Mahakama	
	Hakimu	01
	Karani	01
3	Polisi	03

4	Binafsi	09
5	Biashara	01
6	PSSSF	01
7	KILIMO	01
8	ZIMAMOTO	01
	JUMLA	**46**

Malalamiko **yasiyohusu** vitendo vya Rushwa yalijumuisha sekta Zifuatazo:-

SN	**SEKTA**	**IDADI**
1	Manispaa ya Temeke WEO TAMISEMI	 01 01
2	Mahakama Karani	 01
3	Polisi	02
4	Binafsi	02
5	TRA	01
	JUMLA	**08**

Takwimu za Majalada yaliyotokana na taarifa zilizohusu vitendo vya Rushwa na yanayoendelea na uchunguzi yapo katika mchanganuo ufuatao:-

NA	**KIPENGELE**	**IDADI**
1	Majalada yaliyoanzishwa uchunguzi wa wazi (Open Investigation)	11
2	Majalada yaliyokamilika	06
3	Malalamiko yanayoendelea kuchambuliwa kwa ajili kuanzishwa uchunguzi wa wazi	29

Takwimu za mashitaka.

NA	**KIPENGELE**	**IDADI**
1	Kesi zilizofunguliwa	4

2	Kesi zilizoamuliwa	2
3	Kesi zilizoshinda	2
4	Kesi zinazoendelea Mahakamani	12

USHIRIKIANO NA WADAU

Pia, TAKUKURU (M) Temeke imeweza kushirikiana na wadau mbalimbali kutoka kwenye sekta tofauti, ambapo mafanikio makubwa ya ushirikiano huo yanaendelea kuonekana. Kwa kipindi cha Januari hadi Machi 2023 TAKUKURU imeweza kushirikiana na wadau tofauti kama ifuatavyo:-

NA	MDAU	MAENEO YA USHIRIKIANO	MATOKEO
1	Wananchi	Uelimishaji	Mwamko mkubwa kwa wananchi katika kushiriki kufichua maovu mbalimbali pamoja na utoaji wa taarifa za vitendo vya Rushwa.
2	Wadau wa haki jinai kama Polisi, NPS, Mahakama, Magereza n.k	Uanzishwaji wa jukwaa la haki jinai (w) Kigamboni na vikao kazi shirikishi vya wadau wa haki jinai.	Uboreshaji wa utoaji huduma kwa kila mdau mshirika, hususani katika kusimamia haki.
3	Watumishi wa idara zingine za Serikali na binafsi (Wakuu wa wilaya za Temeke na Kigamboni, Polisi, Zimamoto n.k)	Kushiriki maadhimisho ya siku ya wanawake kiwilaya na kutoa elimu, Kushiriki Usafi wa mazingira kata ya Buza, Kutembelea na kupeleka vifaa mbalimbali kwa watoto wenye mahitaji maalumu kituo cha Yatima kata ya Chamazi na kituo	Kudumisha mahusiano mema kati ya TAKUKURU na taasisi zingine. Kuongeza wadau washirika katika mapambano dhidi ya rushwa. Elimu kufikia idadi kubwa ya wananchi.

		cha watoto yatima cha Amani Foundation-Kigamboni, Maonyesho ya wanawake katika viwanja vya Taifa vya Benjamini Mkapa, Kushiriki maandamano ya kilele cha maadhimisho ya siku ya wanawake kiwilaya na kushiriki maadhimisho ya siku ya wanawake kimkoa katika viwanja vya Mnazi mmoja.	

Maadhimisho ya Siku ya wiki ya Sheria.

Katika maadhimisho ya WIKI YA SHERIA yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Mahakama ya Hakimu mkazi KISUTU, ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Temeke (Temeke na Kigamboni) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliadhimisha siku hiyo kwa kushiriki katika maonyesho kwa kuwaelimisha wananchi jinsi ya kuzuia Rushwa katika maeneo yao, ikiwa ni Pamoja na utambuzi wa vifungu mbalimbali vya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022 waliofika katika banda la TAKUKURU lilokuwa viwanjani hapo.

Maadhimisho ya siku ya wanawake duniani.

Katika maadhimisho ya SIKU YA WANAWAKE DUNIANI tarehe 8 Machi 2023, ofisi ya TAKUKURU (M) Temeke kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliadhimisha siku hiyo kwa kutoa Elimu kwa wananchi walioshiriki maadhimisho hayo Temeke na Kigamboni kuhusiana na Rushwa na jinsi ambavyo kila mwananchi ana wajibu wa kushiriki katika vita hii kubwa ya mapambano dhidi ya rushwa na jinsi ya kutoa taarifa kwa kupiga 113 bila malipo, kutuma barua/barua pepe au kwa kufika katika ofisi zetu.

MIKAKATI KWA KIPINDI CHA APRILI – JUNI 2023

TAKUKURU Mkoa wa Temeke, inatarajia katika robo ya Aprili - Juni, 2023 kuimarisha juhudi za kuzuia rushwa kwa kuongeza ushiriki wa kila mwananchi na wadau katika kukabili tatizo la rushwa katika utoaji wa huduma za jamii na utekelezaji wa miradi

ya maendeleo na kuhamasisha ushiriki katika vita dhidi ya rushwa kupitia Programu ya **TAKUKURU Rafiki** pamoja na nyenzo mbalimbali za uelimishaji ikiwemo vipindi vya redio pamoja na uelimishaji katika mikusanyiko mbalimbali.

Pia tutaendelea kufuatilia makusanyo na uwasilishaji wa mapato yanayotokana na mashine za POS na kuchukua hatua stahiki kwa wale watakaobainika kufuja mali za umma.

Mwisho, tunawashukuru wananchi wa Mkoa wa Temeke na Wilaya ya Kigamboni pamoja na nyie waandishi kwa kutuunga mkono katika vita hii ambayo ni yetu sote. Tunawasihi wengine wote wenye mtazamo kwamba hii ni kazi ya Serikali pekee waachane na fikra hizo batili na wajiunge kuongeza nguvu katika jeshi la wazalendo, waadilifu na wanaojisikia fahari kuzuia rushwa.

Temeke ni njema atakaye na aje.

"KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU"

Imetolewa na:
HOLLE MAKUNGU
Mkuu wa TAKUKURU (M) Temeke
Simu: 0738150239